Ecolebooks.com

JINA……... NAMBARI YAKO……..

DARASA ……... SAHIHI YAKO……..

102/2
KISWAHILI
KARATASI LA PILI
(LUGHA)
DISEMBA 2020
MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA MWIGO WA SUKELLEMO
MTIHANI WA MWIGO 2020

MAAGIZO:

1. Hii karatasi ina kurasa kumi na moja zilizopigwa chapa.
2. Mtahiniwa anapaswa kukagua hii karatasi ili kuthibitisha kuwa kila ukurasa umepigwa chapa na kuwa hakuna swali linalikosekana
3. Jibu maswali yote.
4. Andika majibu katika nafasi uliyotengewa baada ya kila swali.
5. Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili sanifu.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	**80**	

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Miaka mingi ya kutawaliwa na wakoloni iliwafanya wananchi wengi kupuuza umaarufu na uadilifu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa kwa manufaa ya kuarifiana habari mbalimbali kwa ufasaha na kuelewana vyema.

Wakoloni pia waliwashawishi wananchi waone, kwamba lugha ya Kiswahili ni kwa ajili ya watu wale wasiokuwa na elimu na kwa wale ambao hawajastaarabika. Kwa wale wenye 'elimu ya wastaarabu,' wakoloni waliwashawishi kuamini kwamba lugha ya kigeni, yaani Kiingereza, ndiyo hasa lugha inayofaa kwa kujieleza na kufahamishana habari.

Kutokana na vikwazo hivi si ajabu kuona hadi hivi sasa, mwananchi halisi akijitwaza kwamba hawezi kujieleza kwa ufasaha au kumpasha mwenzie habari kwa ukamilifu mpaka atumie lugha ya Kiingereza. Hata katika maofisi mengi ya serikali, hadi hii leo, japo imeshapitishwa kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa bado utawaona wananchi wengine wanapendelea kuzungumza Kiingereza wao kwa wao, ili wajulikane kwamba wana kisomo na wamestaarabika.

Vikwazo vya namna hii vimewalemea wananchi vile vile kwa upande wa magazeti. Utaona mwananchi ambaye anafahamu Kiingereza kidogo sana, akijinunulia gazeti kubwa la Kiingereza na kuanza kuzurura nalo kutwa nzima bila kuambulia mengi ndani yake. Pia utawasikia wananchi wengi wakijidai kwamba hawataki kusoma magazeti ya Kiswahili kwa sababu inakuwa vigumu kwao kuelewa mambo yaliyomo kama vile ambavyo wangelielewa katika gazeti la Kiingereza.

Mabeberu wameshagundua kwamba tunao upotovu wa aina hiyo, ndipo utaona mara nyingi wanawaletea wananchi magazeti mengi ya Kiingereza, mengine yakiwa na nia ya kuwapotosha wakijua kwamba watayasoma tu, mradi yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mara nyingi taifa fulani la kibeberu likitaka tuchukiane na taifa jingine ambalo ni adui yake kisiasa au kiuchumi, taifa hilo la kibeberu linaandika habari za uchochezi kwenye magazeti yao kwa lugha ya Kiingereza, mambo kuhusu taifa lile adui yake (ambalo si adui yetu).

Magazeti hayo huandikwa kwa lugha nadhifu ya Kiingereza na kuletewa wananchi hapa nchini. Maskini wananchi wengine waliotopea kwa kudhani Kiingereza ndicho lugha nzuri ya Kigazeti , wanayanunua mara moja na kuanza kuyasoma magazeti hayo, na pia kuwapa watoto wao wayasome. Matokeo yake ni kwamba, bila kujitambua, wanajikuta wanayafanya yale mabeberu waliyotarajia wayafanye, yaani wanaanza kuchukiana bure na taifa lile ambalo ni adui wa mabeberu hao, lakini si adui zetu. Madhumuni ya kuandika habari kwenye magazeti, ni kutaka kuwafahamisha wasomaji mambo yaliyotokea au

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

yatakayotokea siku hata siku, kwa lugha inayofahamika na kueleweka kwa urahisi bila kumtatiza msomaji. Ikiwa basi ndiyo madhumuni, kuna haja gani kutumia lugha ya kigeni ili kuwaelezea wasomaji wako jambo wangaliweza kuelezwa kwa lugha yao wenyewe ambayo wanaielewa vyema.

Mtu aelezeapo jambo kwa maandishi akitumia lugha yake mwenyewe anaielewa vyema na ambayo pia wasomaji wake wataielewa kwa ukamilifu. Kwa ujumla jambo ambalo mwandishi huyo ataliandika kwa lugha ambayo ni ya asili yake ambayo anaielewa vyema, halitamtatiza msomaji wake ambaye pia anaielewa vyema lugha hiyo.

Maswali

a) Eleza mbinu zinazotumiwa na wakoloni kuwafanya wananchi kuidunisha lugha ya Kiswahili (alama 3)

……

……

……

b) Thibitisha kuwepo kwa ukoloni mamboleo katika habari uliyosoma (alama 4)

……

……

……

……

c) Eleza jinsi wabeberu wanaweza kuzua vurugu katika mataifa mbalimbali (alama 2)

……

……

4. Taja sababu ambayo imewafanya wananchi wengi kupuuza lugha ya Kiswahili (alama 1)

……

……

5. Wakoloni wana mtazamo gani kuhusu lugha ya Kiswahili? (alama 2)

……

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

……

……

6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 3)

i. Uadilifu……..……
ii. Akijitwaza……
iii. Waliotopea ……

2. UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tisho kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira. Hii ni kwa kuwa taka huwa na makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya plastiki, huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali. Mifuko ya plastiki ina madhara zaidi kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati mvua za gharika zinaponyesha. Maji hukosa njia yake ya kawaida ambayo huwa imezibwa na mifuko hii. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwingine ya uhai. Fauka ya haya, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja kutafuta njia na teknolojia ya kuweza kukabiliana na taka ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na rasilmali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhilifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano maji ni rasilmali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo huzalisha maji taka kwa wingi. Rasilmali hii inaweza ikatumiwa kwa uangalifu. Kwa mfano badala ya kutumia bafu ya mnyunyu kuogea, mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelezi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi huu. Wengi kwa kukosa hela za kununua mipira ya viwandani hutumia makaratasi na mifuko ya plastiki kutengeneza mipira wanayoitumia. Hii ni teknolojia endelezi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu. Hutoza ada fulani ya uzoaji, kisha huzipeleka taka hizi kule zitakakobadilishwa ili ziwe na manufaa. Mifuko na mabaki ya plastiki kama vile matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengenezea bidhaa nyingine. Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengenezea bidhaa kama vitabu, katoni, shashi za chooni, magazeti na kadhalika.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kwa kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka nazo ni kama vile mabaki ya vyakula, mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku hizi na hasa sehemu za mjini na katika maeneo ya biashara kama mikahawa, hospitali n.k. Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka hizi ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira nayo ina manufaa kemkem. Kwanza, hugeuza taka ambayo inaweza kuwa hatari na kuifanya iwe yenye manufaa. Kwa hivyo, hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katika bustani.

Maji taka, hasa yanayotumiwa kuoshea vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishiwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa.

Aghalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule, hospitali na kadhalika badala ya kupoteza moto bure inawezekana pakawekwa birika kubwa au tangi la chuma ambalo litatumia moto huo kuchemshia maji ambayo yanaweza kutumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuzitupa dawa hizi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo.Kwa vyovyote vile, si jambo muhali kuwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utunzaji huu huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

MASWALI

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, **fupisha** aya ya kwanza na ya pili.

(Maneno 70) (alama 7,1 ya mtiririko)

Matayarisho

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

(b) Kwa kuzingatia aya ya 3,4,5,6 na 7 **eleza** mambo muhimu anayoshughulikia mwandishi
(maneno 100– 120) (alama 8,1 ya mtiririko)

Matayarisho

……

……

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

3. **SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a. Andika neno moja lilo na mpangilio wa sauti zifuatazo: kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya nyuma wastani. (alama 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

……

……

b. Eleza miundo ya silabi katika neno**: mbilikimo**. (alama 2)

……

……

……

c. Tunga sentensi ya **neno moja** iliyo na vipashio viifuatavyo vya kisarufi: kiima, kiambishi cha wakati ujao, shamirisho kitondo, mzizi, kauli tendea na kiishio. (alama 3)

……

……

……

d. Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi mawili ya kiambishi **i**. (alama 2)

……

……

……

e. "Akisa! Akisa! Mbona huitiki! Njoo hapa upesi!" mama alimwamrisha. (alama 3)
Andika kwa usemi wa taarifa:

……

……

……

f. Waumini wa kweli humcha Maulana kila wakati. (alama 1)
Anza: Maulana…

……

……

g. **Kanusha kwa udogo**: Ndovu huyu alimdhuru nguruwe huyo mchafu. (alama 2)

……

……

h. Andika kunyume: Shamsi alilewa kisha akaukomea mlango wake usiku. (alama 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

……

……..

i. Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu, kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo. (alama 3)

……

……

j. Ziunganishe sentensi zifuatazo kwa kiunganishi cha masharti. (alama 2)

Wakulima watapata mazao mazuri. Wakulima watazingatia kilimo cha kisasa.

……

……

k. Tumia neno '**mpaka**' katika sentensi kama: (alama 3)

a. Nomino ……..

b. Kihusishi ……

c. Kiunganishi ……

l. Bainisha aina za vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kipakatalishi kilichonunuliwa jana kitatumiwa inavyotakiwa na mwenyewe.

……

……

……

m. Ichanganue sentensi ifuatayo kwa visanduku: (alama 3)

Matandiko na Sisomi wataketi karibu na daraja.

……

……

……

……

……

……

……

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

n. Jibu kulingana na maagizo:

i. Kwetu kumenyesha mvua usiku kutwa na waongozi wakahairisha mikakati ya kuthibiti mmomonyoko wa udongo. (Sahihisha) (alama 2)

……

……

ii. Mwanariadha bora alipewa **zawadi** kisha akaandaliwa **karamu** katika ikulu. (Andika upya ukigeuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa vitenzi). (alama 2)

……

……..

o. Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Ajuza huyo alijengewa nyumba kwa matofali na mwanawe mara moja. (alama 2)

……

……

……

……

p. Tunasema simile tunapoomba kupishwa, taib tunapo…….. na ……. tunapotaka kitu kinusurike. (alama 2)

q. Tunga sentensi moja yenye kirai elezi na kirai kihusishi. (alama 2)

……

……

……

r. Jamala ni kwa hisani, kaba ni kwa …….. na …….. ni kwa mziwanda. (alama 2)

s. Iainishe sentensi ifuatayo kwa kuzingatia dhamira. (alama 1)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Meza tembe mbili mara tatu kila siku.

……

……..

4. SEHEMU D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)

a. Fafanua dhana ya wingilugha. (alama 1)

……

……

b. Eleza mambo manne yanayosababisha wingilugha. (alama 4)

……

……

……

……

……

……

……

……

……..…

c. Fafanua sababu tano za watu kuhamisha na kuchanganya msimbo katika mawasiliano. (alama 5)

……

……

……

……

……

……

……

……

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

.....

.....

.....

.....

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM